



ذموات شاداد

MWANAMFALME MNYAMAVU

(Swahili)

Shaikh-e-Tauziqat Ameer-e-AhleSunnat
Mwanuzilishi wa Dawat-e-Islami,
Allama Moulana Abu Bilal

MUHAMMAD ILYAS
Attar Qadiri Razavi رحمۃ اللہ علیہ

حاشیہ شہزادہ

MWANA FALME MNYAMAVU

Kijitabu hiki kiliandikwa na Shaykh-e-Tariqat Amīr-e-Ahl-e-Sunnat, muanzilishi wa Dawat-e-islami 'Allāmah Maulānā Abu Bilal Muhammad Ilyas Attar Qadiri Razavi داعیہ برکاتہم العالیہ

Katika lugha ya Kiurdu. Kimetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili na Majlise Tarajim. Endapo utaona makosa yoyote katika tafsiri yake au utungaji wake, tafadhali wajulishe Majlise Tarajim kwa njia ya posta au kwa kipepesi ili upate thawabu.

Majlise tarajim (Dawat-e-islami)

Alami Madani Markaz, Faizan-e-Madina, Mahalla Saudagran,
Old Sabzi Mandi, Baab-ul-Madina, Karachi, Pakistan
Wasiliana kwa nambari: +92-21-34921389 hadi 91
translation@dawateislami.net

Maktaba-tul-Madina

UK: 80-82 Bordesley Green Road, Birmingham, B9 4TA
Contact #: 07989996380 - 07867860092
Email: uk@dawateislami.net

USA: Faizan-e-Madina, P. O. Box 36216, Houston, Tx 77274
Contact #: +713-459-1581, 832-618-5101

INDIA: 19/20 Muhammad Ali Road, Opposite Mandvi Post Office
Mumbai - 400 003
Contact #: +91-022-23454429

BANGLADESH: K.M Bhovan, 1st Floor, 11, Andar Killa Chittagong.

HONG KONG: Faizan-e-Madina, M/F-75, Ho Pui Street, Tsuen Wan
N.T.
Contact #: +85-98750884 – 31451557

SOUTH AFRICA: 61A, Mint Road, Fordsburg, Johannesburg.
Contact #: 011-838 9099

KENYA: Kanz-ul-Iman, Near Al-Farooq Hospital, Tonoka Area
Mvita, Mombasa
Contact #: +254-721-521916

TORONTO CANADA: 1060 Britannia Road Unit 20, 21 Mississauga
ONT Canada
Contact #: +141-664-82261

الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ وَالصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ عَلَى سَيِّدِ الْمُرْسَلِينَ
أَمَّا بَعْدُ فَأَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Dua kabla ya kusoma kitabu

Kabla ya kusoma kitabu au somo la kidini, soma dua ifuatayo.
Insha-Allah عَزَّوَجَلَّ utakumbuka yote uliyoyasoma.

اللَّهُمَّ افْتَحْ عَلَيْنَا حِكْمَتَكَ وَاَنْشُرْ
عَلَيْنَا رَحْمَتَكَ يَا ذَا الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ

Ee mola عَزَّوَجَلَّ Ifungue milango ya elimu na busara kwa ajili yetu,
na utuhurumie! Ewe ulie mtakatifu kabisa.

(Al-Mustatraf, Vol. I, p. 40, Dar-ul-Fikr, Beirut)

Kumbuka: Mswalie Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ mara moja kabla na
baada ya dua. *(Roohani Hikiyat UK. 68)*

Orodha Ya Yaliyomo

MWANAMFALME MNYAMAVU

Ubora wa kumsalia mtume ﷺ	1
Kunyamaza huleta usalama	2
Bahram na ndege.....	2
Hadithi nne kuhusu ubora wa ukimya.....	3
Ufafanuzi wa 'ni bora kuliko ibada ya miaka 60'	3
Madhara manne ya kuropoka	3
Kitu chenye madhara zaidi	5
Ima sema neno jema au nyamaza.....	5
Ikiwa wataka pepo, basi.....	6
Kunyamaza ni njia ya kuihifadhi imani	6
Kunyamaza ni stara ya mjinga.....	7
Kunyamaza ni ufunguo wa ibada.....	7
Ni rahisi kulinda mali, lakini ulimi... ..	7
Aropokaye hujijutia.....	8
Kujuta baada ya kunyamaza ni bora kuliko kujuta baada ya kuropoka .	8
Bubu yu salama zaidi	9
Nyumba huwaje mahala pa amani?	9
Tiba ya kimadani ya kusuluhisha migongano ya mama mkwe na mavyya	10

Ombi (la viungo) kwa ulimi.....	10
Uboru wa kusema mazuri	11
Mtume ﷺ alikuwa akikaa kimya muda mrefu	11
Aina mbili za kuzungumza na kunyamaza	12
Ufafanuzi wa mazungumzo machafu	13
Damu na usaha zitatoka midomoni mwao	14
Atafufuliwa kwa sura za jibwa	15
Ameharamishiwa pepo.....	15
Shada lenye maua saba la Al Faruq.....	15
Laiti ingekuwa hivi.....	16
Siri ya swahaba kuwa mtu wa peponi.....	16
Mifano ya mazungumzo ya upuuzi	17
Ni vigumu kwa mropokaji kujizuia na dhambi za kuongeza chumvi urongo.....	19
Laiti tungeli subiri na kupima tunachotaka kuzungumza tungelipata baraka	20
Mazungumzo kuhusu ugaidi yasiyo na maana	20
Siddiq akbar alikuwa akiweka kijiwe mdomoni	21
Kufanya mazoezi ya kunyamaza kwa miaka arobaini.....	22
Tabii (mtu aliyesubiana na swahaba) aliyekuwa akijitathmini mazungumzo yake ya kila siku	22
Namna ya kutathmini mazungumzo.....	23
‘Umar bin ‘abdu ‘aziz alia kwa shaki	24
Maelezo ya kisa hiki	24

Tiba bora zaidi ya kutakasa mazungumzo na maneno yasiyokuwa na maana.....	25
Mjinga husema bila ya kufikiria.....	27
Mbinu ya kupima (maneno) kabla ya kusema.....	27
Mbinu ya kunyamaza kimya	28
Itaneni kwa njia ya heshima ili mupate thawabu	30
Baraka Tatu Zitokanazo na Kunyamaza	31
1. Kumuona mtume Mtukufu ﷺ kwa sababu ya baraka ya kunyamza	31
2. Faida ya kunyamaza katika kuimarisha mazingira ya Madani ...	32
3. Faida ya kunyamaza katika kuimarisha mazingira ya Madani nyumbani	34
Maua ya madani 19 ya kuimarisha mazingira ya nyumbani	35
20 faida za madani kuhusu mswaki.....	39
Amali inayosababisha kupungua kwa adhabu	43
Msamaha kwa aliyeabudu moto.....	46

الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ وَالصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ عَلَى سَيِّدِ الْمُرْسَلِينَ
أَمَّا بَعْدُ فَأَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

MWANAMFALME

MNYAMAVU

Ijapokuwa shetani atataka kukuzuia kusoma kitabu hiki, kisome chote. Ikiwa ulikuwa si muangalifu katika kuutumia ulimi wako, utatokwa na machozi bora tu moyo wako una hofu ya Mwenyezimungu عَزَّوَجَلَّ.

Ubora Wa Kumsalia Mtume ﷺ

Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ ambaye ni pozo la nyoyo zetu, mkarimu na mpole amesema, “Kumtaja Mwenyezimungu عَزَّوَجَلَّ kwa wingi na kuniswalia mimi huondoa ufukara.” (*Al-Qawl-ul-Badi*, uk. 273)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Mara mwanafalme akanyamaza. Watu wote; akiwemo mfalme mwenyewe, mawaziri na wengineo hawakujuwa kilichompata mwana yule. Kila mtu alijaribu kumzungumzisha lakini hakuna aliyefaulu. Japo alikuwa mkimya sana, shughuli zake za

nyumbani aliziendeleza kama kawaida. Siku moja alikwenda kuwinda ndege na wenzake msituni. Alipokuwa chini ya mti huku amejihami kwa uta na mishale akitafuta ndege, mara akasikia mperekecho wa utagaa kutoka sehemu fulani, hapo hapo akafuma mshale upande wa sauti na akamlenga ndege. Yule ndege alianguka na kugaa gaa kwa maumivu. Kwa ghafla bila ya watu kutarajia, yule mwanmfalme akasema, “Huyu ndege alipokuwa amenyamaa alikuwa salama lakini alipotamka tu akaangamizwa na mshale wangu. Na ni jambo la kusikitisha kuwa alipozungumza nami ikanibidi nizungumze.”

Kunyamaza Huleta Usalama

Ndugu wapenzi waislamu! Ingawa kisa hiki kimebuniwa lakini ni ukweli usiopingika kwamba mropokaji huwafanya wengine pia kuzungumza, hupoteza wakati wake na wakati wa wenziwe, tena hujutia aliyoyasema na hupata matatizo mengi. Bila shaka mtu akiwa amekaa kimya, huepukana na balaa nyingi.

Bahram Na Ndege

Imepokewa kuwa Bahram alikuwa amekaa chini ya mti mara akasikia sauti ya ndege. Alimfuma ndege huyo, halafu akasema; “Kuulinda ulimi ni faida kwa binadamu na ndege. Lau ndege huyu angeulinda ulimi wake hangeangamia.” (*Mustatraf, uk. 147, juz 1*)

Hadithi Nne Kuhusu Ubora Wa Ukimya

1. مَنْ صَمَّتْ نَجَا “Mwenye kunyamaza ameokoka.” (*Sunan-ut-Tirmiḏī, uk. 225, juz. 4, hadith 2509*)
2. الصَّمْتُ سَيِّدُ الْأَخْلَاقِ “Kunyamaza ndiyo kiongozi wa maadili yote.” (*Al-Firdaws bimā Ṣawr-ul-Khaṭṭāb, uk. 417, juz. 2, hadith 3850*)
3. الصَّمْتُ أَرْفَعُ الْعِبَادَةَ “Kunyamaza ni ibada ya daraja ya juu.” (*Al-Firdaws, hadith 3849*)
4. “Mtu kuwa na msimamo juu ya ukimya ni bora kuliko kufanya ibada miaka 60.” (*Shu’ab-ul-Īmān, uk. 245, juz. 4, hadith 4953*)

Ufafanuzi Wa 'Ni Bora Kuliko Ibada Ya Miaka 60'

Mfasiri mkubwa wa Quran aitwaye Ḥakīm-ul-Ummat, Mufti Aḥmad Yār Khān Na’imī رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى عَلَيْهِ ameandika kuhusu hadithi hii ya nne: “Lau mtu atafanya ibada miaka sitini lakini husema sana na hatofautishi baina ya mazungumzo mazuri na mabaya basi ni bora kunyamaa kidogo kwani ndani ya ukimya kuna kuzingatia, muna utambuzi na marekebisho ya nafsi, muna kuzama ndani ya bahari ya kumtaja Mwenyezimungu عَزَّ وَجَلَّ moyoni na muna kuvuta fikra.” (*Mirāt-ul-Manājih, uk. 361, juz. 6*)

Madhara Manne Ya Kuropoka

Wale wanaoropoka, wanaozusha ugomvi katika mazungumzo huku wakidhani kwamba kuzungumza ovyo ovyo inaruhusiwa

na si dhambi wanafaa kuzingatia mtazamo wa Hujjat-ul-Islam Sayyidunā Imām Muhammad Bin Muhammad Bin Muhammad Ghazālī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْوَالِي kuhusu mazungumzo yasio na faida na wanafaa kuogopa kutokana na madhara haya manne:

1. Kirāman Kātibīn (malaika wa kuandika amali) huwabidi kuandika mazungumzo yasio na faida. Kwa hivyo yafaa mtu awaonee haya na asiwape tabu ya kuandika maneno ya kipuuzi. Allah عَزَّوَجَلَّ katika aya 18 surah Qāf anasema:

مَا يَلْفِظُ مِنْ قَوْلٍ إِلَّا لَدَيْهِ رَقِيبٌ عَتِيدٌ ﴿١٨﴾

Hatoi kauli yoyote isipokuwa
karibu naye yuko mngojeaji tayari (kuandika).

2. Ni aibu iliyoje maneno ya upuuzi yaliyorekodiwa kuletwa mbele ya mahakama ya Allah عَزَّوَجَلَّ!
3. Katika mahakama ya Allah عَزَّوَجَلَّ, mja atasimamishwa mbele ya viumbe vyote na kuamrisha kusoma kitabu chake cha amali! Utisho wa siku ya kiyama utakuwa mbele yake, atakuwa uchi, ana kiu kali, mgongo umepinda na kukaribia kuvunjika kwa sababu ya njaa, atazuiliwa kuingia peponi na atanyimwa kila aina ya raha. Hebu tufikirie itakuwa dhiki ilioje mtu kuambiwa asome kitabu chake cha amali kilichojaa maneno ya upuuzi katika hali hiyo! (Tufanye hisabu, kwa dakika 15 za maneno ya upuuzi kwa siku moja ni kama masaa 7 1/2 katika mwezi mzima; ambayo ni sawa na masaa 90

kwa mwaka mzima. Ikiwa mtu ataishi miaka 50 na kila siku awe atazungumza maneno ya upuuzi kwa dakika 15 basi zitakuwa siku 187 na masaa 12 yani itakuwa ni zaidi ya miezi sita. Sasa fikiri katika hadhara hii ambapo jua limeteremshwa kufikia utosini nani ataweza kuyasoma maneno yake ya upuuzi kwa mfululizo kwa zaidi ya miezi sita! Huu ni mfano wa maneno ya upuuzi kwa dakika 15 kila siku. Wakati mwengine sisi hupoteza masaa na rafiki zetu katika maneno ya upuuzi. Mbali na hayo kuna mazungumzo ya madhambi na maovu mengine juu yake!)

4. Siku ya Kiyama mtu atalaumiwa na kuaibishwa kutokana na maneno yake ya upuuzi. Atakuwa hana la kujitetea mbele ya Allah **عَزَّوَجَلَّ**. Ataroa jasho kwa ajili ya kuona aibu. *(Minhāj-ul-‘Ābidīn, uk. 67)*

Kitu Chenye Madhara Zaidi

Sayyidunā Sufyān Bin ‘Abdullāh **رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ** amesema, “Siku moja nilimuuliza Mtume **صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ** ni kitu gani chenye madhara zaidi kwangu? Mtume mpendwa **صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ** akashika ulimi wake na akaniambia, “Huu.” *(Sunan-ut-Tirmizī, uk. 184, juz. 4, hadith 2418)*

Ima Sema Neno Jema Au Nyamaza

Laiti hadithi hii ya Bukhari Sharif ingekaa vizuri katika akili zetu, **“مَنْ كَانَ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ فَلْيَقُلْ خَيْرًا أَوْ لِيَصْمُتْ**”

kumuamini Allah **عَزَّوَجَلَّ** na Siku ya Kiyama, ima aseme (neni) zuri au anyamaze.” (*Ṣaḥīḥ Bukhārī, uk. 105, juz. 4, hadith 6018*)

Katika kitabu ‘*Allah-Wālon kī Bātayn*’ chenye kurasa 217 kilichochapishwa na Maktaba-tul-Madinaḥ, katika ukurasa wa 91, Amīr-ul-Mūminīn Sayyidunā Ṣiddīq Akbar **رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ** amesema, “Hapana uzuri wowote katika mazungumzo yasiyokuwa ya kumfurahisha Allah **عَزَّوَجَلَّ**.” (*Hilya-tul-Awliyā, uk. 71, juz. 1*)

Sayyidunā Imām Sufyān Ṣaurī **رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ** amesema, “Ngazi ya kwanza ya ibada ni kunyamaza, ya pili ni kupata ilimu, halafu kuihifadhi, halafu kuifanyia amali, na halafu kuwaelezea wengine.” (*Tarīkh-ul-Baghdad, uk. 6, juz. 6*)

Ikiwa Wataka Pepo, Basi...

Watu walimwendea Sayyiduna ‘Isa **عَلَى نَبِيِّنَا وَ عَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَام** na wakamuuliza, “Tuambie ni amali gani ambayo kwayo tutaingia peponi?” Akajibu, “Musiseme kabisa.” Wakamuambia, “Hilo haliwezekani.” Akajibu, “Basi musiseme chochote kwa ulimi wenu ila la kheri tu.” (*Iḥyā-ul-‘Ulūm, uk. 136, juz. 3*)

Kunyamaza Ni Njia Ya Kuihifadhi Imani

Mwenye kudaka au kukata kauli mwenzake hubakia katika kutomuelewa mwenzie na pia maneno ya kufuru yanaweza kupenya ulimini mwake. Ḥujjat-ul-Islam Sayyidunā Imām Muhammad Bin Muhammad Bin Muhammad Ghazālī **عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللهِ الْوَالِي** amesema

katika Ihyā-ul-‘Ulūm kwamba sifa mbili hubakia nazo mwenye kunyamaza:

1. Dini yake huwa madhubuti
2. Humuelewa vizuri anayezungumza naye. (*Ihyā-ul-‘Ulūm, uk. 137, juz. 3*)

Kunyamaza Ni Stara Ya Mjinga

Sayyidunā Sufyān Bin ‘Uyaynāh رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ amesema, “Kimya ni heshima ya mwanachuoni na ni stara ya mjinga.” (*Shu’ab-ul-Īmān, uk. 86, juz. 7, hadith 4701*)

Kunyamaza Ni Ufunguo Wa Ibada

Imepokelewa kutoka kwa Sayyidunā Imām Sufyān رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ, “Kukaa kimya sana ndio ufunguo wa ibada.” (*Aṣ-Ṣamt ma’ Mawsū’ah Ibn Abid-Dunyā, uk. 255, juz. 7, hadith 436*)

Ni Rahisi Kulinda Mali, Lakini Ulimi...

Sayyidunā Muhammad Bin Wāsi’ عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ alimwambia Sayyidunā Mālik Bin Dīnār عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ, “Mtu kulinda ulimi ni ngumu zaidi kuliko kulinda mali.” (*Ithaf-us-Sādat-liz-Zubaydī, uk. 144, juz. 9*)

Ni jambo la kusikitisha kwamba kila mtu yuko chonjo kulinda mali ingawa mali ikipotea ni hasara tu ya dunia. Bila shaka matokeo ya kutolinda ulimi sambamba na hasara ya dunia pia kuna hatari kubwa ya kupata shida kesho akhera.

Aropokaye Hujjutia

Ndugu waislamu! Ni dhahiri kuwa katika kuzungumza kuna nafasi kubwa ya kuaibika kuliko kunyamaza. Mzoefu wa kuropoka mara nyingi hubidi kuomba msamaha au hujuta moyoni, “Kama nisingezungumza wakati ule, ingekuwa bora; kwa sababu ya kuzungumza kwangu thamani yangu ikapotea na akanifokea, fulani akaudhika, fulani akawa hana raha, heshima yangu ikadhurika nakadhalika.” Imepokelewa kutoka kwa Muhammad Bin Naḍr Ḥārīṣī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْقَوِي, “Heshima hupotea kwa kuropoka.”
(Aṣ-Ṣamt ma' Mawsū'ah Ibn Abid-Dunyā, uk. 60, juz. 7, hadith 52)

Kujuta Baada Ya Kunyamaza Ni Bora Kuliko Kujuta

Baada Ya Kuropoka

Ni kweli kwamba ni bora kujuta baada ya kunyamaza kuliko baada ya kuzungumza na ni bora kujuta baada ya kula kidogo kuliko baada ya kula sana, kwani anayeropoka hupata matatizo; na anayekula sana huharibu tumbo lake. Kawaida hunona kupita kiasi na hupata maradhi mengi ima katika ujana wake au uzee wake. Ukitaka kujua zaidi kuhusu madhara ya kula kupita kiasi, soma kitabu *Faizan e Sunnat* juzuu 1 sura *Faida Za Njaa*.

Bubu Yu Salama Zaidi

Ndugu wapenzi waislamu! Mukimuangalia kipofu mutaona amesalimika kutokana na madhambi ya kuangalia kama vile kuwaangalia wanawake anaofaa kuwaoa, vijana wazuri kwa matamano, filamu na drama, magoti na mapaja ya mtu aliyevaa suruali fupi. Vilevile bubu pia amesalimika kutokana na balaa nyingi za ulimi.

Amīr-ul-Mūminīn Sayyidunā Abū Bakr Ṣiddīq رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ amesema, “Afadhali ningekuwa bubu na ningepewa tu nafasi ya kumtaja Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ.” (*Mirqāt-ul-Mafātīh*, uk. 87, juz. 10, *hadith 5826*)

Sayyidunā Abū Dardā رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ alimuona mwanamke asema sana. Akasema, “Ingekuwa bora kwake kama angekuwa bubu.” (*Iḥyā-ul-‘Ulūm*, uk. 142, juz. 3)

Nyumba Huwaje Mahala Pa Amani?

Kutokana na maneno ya swahaba huyu رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ kina dada zetu ambao huzungumza porojo na hawachoki kusema hili na lile wangepata funzo.

Ikiwa kina dada waislamu watafunga Qufl-e-madinah kisawasawa basi matatizo yao ya kinyumbani, kukosana na familia, ugomvi kati ya mke na mkwewe na migogoro mengine yangeisha na majumba yangekuwa mahali pa amani. Kwa sababu matatizo mengi ya kinyumbani husababishwa na ulimi.

Tiba Ya Kimadani Ya Kusuluhisha Migongano Ya

Mama Mkwe Na Mavyaa

Ikiwa mama mkwe atamfokea mavyaa wake basi mavyaa afaa anyamaze na avumilie na asiseme hata neno moja kumjibu wala kuenda kumsema kwa mumewe au kwa wazazi wake, wala asikunje uso au kuelekeza hasira zake kwa watoto au kwa vyombo. **إِنَّ هَذَا لِلَّهِ عَزَّوَجَلَّ** atapata mafanikio makubwa. Inasemekana, “Kunyamaza mara moja hushinda watu mia.” Vile vile ikiwa mavyaa atagombana na mama mkwe basi mama mkwe asimjibu bali anyamaze kimya, asimshtakie mtu yeyote katika familia hata mwanawe. Kutokana na msembo, “Kunyamaza mara moja huleta utulivu mara mia” **إِنَّ هَذَا لِلَّهِ عَزَّوَجَلَّ** atapata utulivu. Ikiwa tiba hii ya KiMadani itazingatiwa kisawasawa basi ugomvi wowote kati ya mama mkwe na mavyaa utasuluhishwa haraka na nyumba **إِنَّ هَذَا لِلَّهِ عَزَّوَجَلَّ** itakuwa mahali penye amani. Ili kupata tiba ya migongano kati ya mama mkwe na mavyaa tazama VCD iitwayo ‘*Ghar Aman kā Gahwārah Kaysay Banay*’ kutoka Maktaba-tul-Madīnah. Kutokana na baraka ya VCD hii nyumba nyingi zilizokuwa na migogoro zimegeuka na kuwa na amani.

Ombi (La Viungo) Kwa Ulimi

Ndugu wapenzi waislamu, ulimi ukiongoka na ukitumika kusema mazuri tu pekee basi mwili mzima utafaidika kwayo na ukiwa kombo, kwa mfano ukitumika kutukana, kuadhirisha, kusengenya au kumchimba mtu au kusema uongo basi wakati mwengine hata katika ulimwengu huu mwili hupata madhara.

Mtume wa rahma na shafii wa umma mmiliki wa pepo صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema, “Binadamu anapoamka asubuhi viungo vyake vyote huuomba ulimi na kuuambia, “Mche Mola kwa ajili yetu kwa sababu sisi tunashirikiana na wewe. Wewe ukiwa sawasawa nasi tutakuwa sawasawa, lakini ukipotoka nasi tutapotoka. (Sunan-ut-Tirmizī, uk. 183, juz. 4, hadith 2415)

Ubora Wa Kusema Mazuri

Mtume mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema, “Peponi kuna roshani ambazo nje yake yaonekana kutoka ndani; na ndani yake yaonekana kutoka nje.” Akaulizwa na Bedui mmoja, “Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu “Ni za kina nani (roshani hizo)?” Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akajibu, “Hizi ni za yule asemaye mazuri, alishaye wengine, afungaye sana, na ainukaye usiku kusali kwa ajili ya Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ ilhali watu wamelala.” (Sunan-ut-Tirmizī, uk. 237, juz. 4, hadith 2535)

Mtume ﷺ Alikuwa Akikaa Kimya Muda Mrefu

كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ طَوِيلَ الصَّمْتِ

Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alikuwa akikaa kimya kwa muda mrefu. (Sharḥ-us-Sunnah-lil-Baghawī, uk. 45, juz. 7, hadith 3589)

Mfasiri mkubwa Ḥakīm-ul-Ummat, Mufti Aḥmad Yār Khān عَلَيْهِ رَحْمَةُ الْمَلَأَن akiielezea hadithi hii, maana ya ukimya huu ni

ule wa kutozungumzia mambo ya kilimwengu ila alikuwa akimtaja Allah ﷺ na hazungumzi na watu ila kwa dharura na akizungumza huwa ni mazungumzo yanayofaa. Daima maneno ya uongo, usengenyaji na fitina hayakupata nafasi ndani ya kinywa kitukufu cha Mtume ﷺ. Yeye mwenyewe ni ukweli vipi ataandamwa na uongo! (*Mirāt-ul-Manājih, uk. 81, juz. 8*)

Aina Mbili Za Kuzungumza Na Kunyamaza

Mtume mtukufu ﷺ amesema:

إِمْلَاءُ الْخَيْرِ خَيْرٌ مِّنَ السُّكُوتِ وَالسُّكُوتُ خَيْرٌ مِّنْ إِمْلَاءِ الشَّرِّ

“Kusema mazuri ni bora kuliko kunyamaza, na kunyamaza ni bora kuliko kusema mabaya.” (*Shu’ab-ul-Īmān, uk. 256, juz. 4, hadith 4993*)

Sayyidunā ‘Alī Bin ‘Ushmān Ḥajwaīrī, ajulikanaye kama ‘Dātā Ganj Bakhsh’ رحمه الله تعالى عليه aliandika katika kitabu chake *Kashf-ul-Mahjūb*: Kuzungumza ni kwa aina mbili, kuzungumza ukweli na kuzungumza uongo. Vilevile kunyamaza ni kwa ‘aina mbili:

1. Kunyamaza kwa lengo (kwa mfano kunyamaza ili kufikiria mambo ya akhera au hukumu za dini)
2. Kunyamaza kwa kughafilika (mfano kuwaza mambo machafu au ya kiduniya yasiyokuwa na faida).

Mtu yeyote aliyenyamaza afikirie vizuri, ikiwa maneno yake ni ya haki basi ni bora kusema kuliko kunyamaza na ikiwa maneno yake ni ya batili basi kunyamaza ni bora kuliko kusema. Sayyidunā Dātā Ganj Bakhsh رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى عَلَيْهِ akatoa kisa kwamba Sayyidunā Abū Bakr Shibli Baghdadi عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْهَادِي alikuwa akipita mtaa fulani katika mji wa Baghdad na akamsikia mtu akisema, اَلشُّكُوتُ خَيْرٌ مِنَ الْكَلَامِ, “Kunyamaza ni bora kuliko kusema.” Akamwambia, “Kwako wewe, kimya chako ni bora kuliko kusema lakini kwangu mimi kusema ni bora kuliko kunyamaza.”

(Kashf-ul-Mahjūb, uk. 402)

Ufafanuzi Wa Mazungumzo Machafu

Ni bahati nzuri ilioje kwa ndugu zetu waislamu ambao hutumia ndimi zao kwa mazungumzo ya adabu na kuwalingania watu katika mambo mazuri. Kwa bahati mbaya si rahisi siku hizi kupata mjumuiko wa watu ambao hauzungumzii mambo machafu. La kushangaza ni kwamba hata wale ambao wanaonekana kuwa na haiba ya nje ya dini wameshindwa kujizuia kuzungumza maneno machafu. Pengine hawaelewi mazungumzo machafu ni yapi. Ufafanuzi wa mazungumzo machafu ni:

التَّعْبِيرُ عَنِ الْأُمُورِ الْمُسْتَقْبَحَةِ بِالْعِبَارَاتِ الصَّرِيحَةِ

Kutaja mambo ya aibu waziwazi

(Ihyā-ul-'Ulūm, pp. 151, vol. 3)

Wale vijana wenye kuchochea mazungumzo kuhusu ngono na maneno yanayotakikana kuhifadhiwa katika ndoa kwa ajili ya kutosheleza uchu wao, wale wanaojipumbaza nafsi zao kwa kuzungumzia au hata kusikiliza mazungumzo machafu, wale wanaotoa matusi, wale wanaotumia ishara chafu, wale wanaopata raha kutokana na ishara hizi na wale wanotazama filamu na drama ili kutosheleza matamania machafu (kwa sababu kuna uchafu mwingi katika filamu na drama hizi) wasome kila mara riwaya ifuatayo yenye kutingisha moyo na wamche Mwenyezimungu عَزَّوَجَلَّ.

Damu Na Usaha Zitatoka Midomoni Mwao

Imepokewa kwamba watu aina nne wa jahannam watakuwa wakihangaika katikati ya moto na maji moto, huku wakiomba kuangamizwa kabisa (ili adhabu ile iwaepuke). Mmoja kati yao atakuwa akitokwa na damu na usaha mdomoni hata wale wenziwe motoni watasema, “Mtu huyu muovu amefanya nini hata atuongeze adhabu zetu?” Jibu litasema, “Muovu huyu alikuwa akipenda kusikiliza na kufurahikia mazungumzo machafu kuhusu kujamiiana. (*Ithaf-us-Sadat-liz-Zubaydi, pp. 187, vol. 9*)uk. 187, juz. 9).

Basi wale ambao wanajishughulisha na mawazo machafu ya kishetani kuhusu wanawake na wavulana wadogo wazuri na huona raha na mawazo mabaya yafaa wazingatie riwaya hii.

Atafufuliwa Kwa Sura Za Jibwa

Sayyidunā Ibrāhīm Bin Maysarah رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ amesema, “Mwenye kuzungumza maneno machafu atafufuliwa siku ya kiyama kwa sura za jibwa.” (*Ithaf-us-Sādat-liz-Zubaydī, uk. 190, juz. 9*)

Ameharamishiwa Pepo

Mtume wa rehma, shafii wa ummah na utulivu wa moyo صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema, “Ameharamishiwa pepo mtu ambaye hutoa maneno machafu.” (*Aṣ-Ṣamt ma' Mawsū'ah Ibn Abid-Dunyā, uk. 204, juz. 7, hadith 325*)

Shada lenye maua saba la Al Fārūq

Amīr-ul-Mūminīn Sayyidunā ‘Umar Fārūq A’zam رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهَا amesema:

1. Mwenye kujiepusha na kusema upuuzi hubarikiwa ilimu na busara.
2. Mwenye kujiepusha na kuangalia angalia ovyo ovyo atapata utulivu wa moyo.
3. Mwenye kujizuia kula ovyo ovyo (kula sana, kula bila ya kuwa na njaa) hupata utamu katika ibada.
4. Mwenye kujizuia na kuchekacheka hupata haiba.
5. Mwenye kujizuia na dhihaka nyingi na stihzai hupata mwanga wa imani.

6. Mwenye kujiepusha na kuupenda ulimwengu hupawa mapenzi ya akhera.
7. Mwenye kujizuia na kuangalia makosa ya wengine hubarikiwa na uwezo wa kurekebisha makosa yake.
(Al-Munabbihāt, uk. 89)

Laiti Ingekuwa Hivi...

Ndugu muislamu! Fanya uradi wa kukisoma kitabu hiki kila Jumatatu ya kwanza ya mwezi wa kiislamu. **إِنْ شَاءَ اللَّهُ عَزَّوَجَلَّ** utaona tofauti kubwa katika maisha yako. Njia bora ya kuzikinga ndimi zetu ni kufuata Madani Inaam 45 na 46. Ili kupata mazoea ya kujiepushe na mazungumzo ya upuuzi yafupishe maneno. Na zaidi jaribu kuwasiliana na watu kwa kutumia ishara na maandishi. Iwapo ulimi utateleza basi mswaliye Mtume **صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ** mara moja au tatu papo hapo.

Siri Ya Swahaba Kuwa Mtu Wa Peponi

Mtume **صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ** kwa idhini ya Mwenyezi Mungu **عَزَّوَجَلَّ**, alibarikiwa uwezo wa kujua iwapo mtu atakwenda peponi au motoni. Siku moja Mtume **صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ** alisema, “Mtu wa kwanza atakayeingia mlango huu atakwenda peponi.” Mara Sayyidunā ‘Abdullāh Bin Salām **رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ** akapita na watu wakampongeza. Halafu wote wakamuuliza, “Umepata bahati hiyo kwa amali gani?” Akasema, “Matendo yangu ni machache na matendo ambayo kwayo natarajia kwa Mwenyezi Mungu ni

kuulinda moyo wangu na ninajiepusha na mazungumzo ya upuuzi.” (*Aṣ-Ṣamt ma' Mawsū'ah Ibn Abid-Dunyā, uk. 86, juz. 7, hadith111*)

Maana ya ‘kuulinda moyo’ ni kutakasika kwa moyo na mambo ya upuuzi na maradhi mabaya (kama wivu) na kuwa na imani thabiti.

Mifano Ya Mazungumzo Ya Upuuzi

Ndugu waislamu wapenzi, ingawa mazungumzo ya upuuzi si dhambi lakini hayana faida yoyote. Sayyidunā ‘Abdullāh Bin Salām رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ alibashiriwa pepo na Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Miongoni mwa sifa nzuri alizokuwa nazo ni kujiepusha kusema maneno ya upuuzi na kuuliza maswali kuhusu mambo yasiyomhusu. Lakini la kusikitisha ni kwamba sisi tunajishughulisha kuuliza maswali ya upuuzi kuhusu mambo yasiyotuhusu ndewe wala sikio. Kwa mfano:

- ❖ Hiki umenunua pesa ngapi?
- ❖ Umekipata kwa pesa ngapi kile?
- ❖ Sehemu fulani na fulani nyumba ni bei gani?
- ❖ Ukitembelea mtu nyumbani kwake au mtu kama amenunua nyumba mpya basi maswali huwa kama yafuatayo:
- ❖ Umenunua bei gani?
- ❖ Ina vyumba vingapi?

- ❖ Kodi yake ni ngapi?
- ❖ Mwenye nyumba yukoje? (swali hili huzua kusengena kwasababu jibu lake bila ya kuzingatia sheria hujibiwa hivi: “ Mwenye nyumba ana roho mbaya/wazimu/ufisadi/ unyama/ugumu nk.
- ❖ Katika muktadha kama huo mtu akinunua duka jipya, gari au piki piki basi maswali yataulizwa kuhusu bei yake, umadhubuti, iwapo kimenunuliwa kwa mkopo au kimelipiwa kwa pesa taslimu.
- ❖ Baadhi ya watu wasiokuwa na busara wakimtembelea mgonjwa mahututi ambaye hata hawezi kuzungumza humuuliza maswali kama ambao wao ni madaktari mahiri na hutaka kujua kwa kina kuhusu repoti ya picha ya x-ray, majaribio ya maabara na iwapo kumekuwa na upasuaji na kama ulikuwako basi ameshonwa vitango vingapi. Hata kama maradhi yanahusu sehemu za siri, watu hawa wasio na haya hutaka kujua kila kitu waziwazi bila kusita. Wanawake nao hawakuachwa nyuma kuhusu mazungumzo yasiyo na faida.
- ❖ Hoja na mijadala isiyo na maana hutolewa kuhusu hali ya anga. Kwa mfano katika majira ya joto, watu wajinga watalalamika, “Siku hizi kuna joto! Na stima nazo hupotea mara kwa mara.”

- ❖ Katika majira ya baridi, watajifanya meno yatetema na watasema, “Leo twaganda kwa baridi kali.”
- ❖ Kama kuna mawingu, basi mtu atatoa hoja isiyokuwa na maana kama siku hizi kuna mvua nyingi. Maji yamejaa kila mahali. Baraza husika halishughuliki kuondoa matope nk.
- ❖ Hoja zisizo na maana kuhusu siasa za nyumbani na za dunia hutolewa bila ya lengo la kuleta mabadiliko na pia vyama vya kisiasa mbali mbali hukosolewa.
- ❖ Ikiwa mtu amezuru miji au nchi nyingine, huanza kuelezea bila kuulizwa mandhari ya milima na mashamba aliyoyaona au maelezo ya nyumba na barabara.
- ❖ Lakini tutanabahi kuwa tukimpata mtu azungumzia mada kama hizo tusimdhania vibaya kwani kuzungumzia mambo ya kidunia kwa nia njema ni thawabu au kwa uchache haihesabiwi kuwa mazungumzo ya upuuzi.

Ni Vigumu Kwa Mropokaji Kujizuia Na Dhambi Za Kuongeza Chumvi Urongo

Liweke akilini kwamba kusema ovyo ovyo si dhambi bora tu iwe ni ukweli ambao haukutiwa chumvi au kupunguzwa chumvi. Ikiwa urongo utatiwa chumvi basi itakuwa ni dhambi. Lakini ni vigumu sana kupima iwapo mtu amepita mipaka ya kusema upuuzi. Kwa watu ambao huzungumza ovyo ovyo kawaida

hutia chumvi katika usemi na huangukia kusengeny, kutafutana makosa na kuwaudhi wengine. Hivyo basi usalama hususan hupatikana katika ukimya kwa sababu ‘Kunyamaza mara moja huleta utulivu mara mia’

Laiti Tungeli Subiri Na Kupima Tunachotaka

Kuzungumza Tungelipata Baraka

Lau mtu angekuza tabia ya ‘kupima maneno’ yaani kufikiria kwa makini kabla ya kuzungumza, basi ataanza kugundua mwenyewe maneno mengi yasiyo na maana. Ikiwa ni ‘mazungumzo yasiyo na maana’ ingawa si dhambi, bado kuna madhara mengi kutokana nayo. Kwa mfano kujisumbua kutumia ulimi na kupoteza wakati muhimu. Ikiwa muda huu utatumika kumtaja Mwenyezi Mungu **عَزَّوَجَلَّ** au kusoma dini au kujihusisha na kufunza sunnah, mtu huenda akapata thawabu nyingi.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Mazungumzo Kuhusu Ugaidi Yasiyo Na Maana

Ikiwa kuna sehemu kumetokea tukio la kigaidi, watu hupata jambo la kuzungumzia lisilo na faida na wakati mwengine kujiingiza katika mazungumzo ya madhambi kuhusu tukio hilo. Hulitaja tukio hilo kila mahali na kulitafsiri kichwa chini maguu juu au kujiingiza katika mijadala isiyokuwa na muelekeo. Wakati mwengine kukashifu vyama vya kisiasa au kiongozi bila msingi nk.

Wakati mwingi mazungumzo kama hayo si kwamba hayana maana tu, bali hueneza hofu na uwoga miongoni mwa watu, hukuza uvumi na husababisha fujo kutokea. Nafsi hupata raha kuzungumza na kusikiliza matukio ya milipuko na ugaidi. Wakati mwengine dua hutolewa (kwa dhahiri) ila tu (kwa ndani) hamu ya kupata raha na kufurahia kuzungumzia na kusikiliza mambo hayo ya kutisha imo moyoni.

Laiti tungegundua fitina hii ya nafsi, tungejizuia kupenda kutaja habari kuhusu milipuko na ugaidi. Hata hivyo tusijizuie kuwataja wale waislamu wanaogandamizwa, kuwahurumia walioumia, waliodhurika au waliouwawa, kuzungumza namna wanavyoweza kusaidiwa na kumuomba Mola **عَزَّوَجَلَّ** aregeshe amani na usalama kwani matendo kama hayo hufanya watu kupata thawabu. Hivyo basi mazungumzo kama hayo yanapotokea fikiria kwa makini nia ya mazungumzo hayo ni ipi? Ikiwa utaona kuwa nia ni nzuri basi ni vizuri (kujihusisha na mazungumzo hayo). Lakini mara nyingi lengo la mazungumzo kama hayo ni kupata ladha.

Siddiq Akbar Alikuwa Akiweka Kijiwe Mdomoni

Tukumbuke kwamba ulimi ni neema kubwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu **عَزَّوَجَلَّ** na tutaulizwa kwayo siku ya Kiyama. Kwa hivyo tusiutumie vibaya. Sayyidunā Abū Bakr Şiddīq **رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ** juu ya kubashiriwa pepo alikuwa muangalifu mno kutumia ulimi. Imesemwa katika Iḥyā-ul-‘Ulūm kwamba Sayyidunā Abū Bakr Şiddīq **رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ** alikuwa akiweka kijiwe

mdomoni mwake ili kuuzuia ulimi kusema. (*Ihya-ul-'Ulum, uk. 137, juz. 3*)

Kufanya Mazoezi Ya Kunyamaza Kwa Miaka Arobaini

Ndugu muislamu mpenzi! Ikiwa unataka kujifunza tabia ya kuwa kimya basi yafaa ulizingatie jambo hili kwa makini na ufanye juhudi kubwa lau sivyo itakuwa vigumu kuweka Qufle-Madinah ya ulimi kwa kufanya juhudi nusunusu. Fanya bidii kukuza tabia ya ukimya kwa kujipa hofu ya hasara ya kuutumia ulimi vibaya. **إِنَّ شَاءَ اللَّهُ عَزَّوَجَلَّ** utafaulu. Hata hivyo uwe thabiti kufanya juhudi hizi. Hebu zingatia kisa cha mtu aliyefanya juhudi kwa istiqama.

Sayyidunā Arṭāḥ Bin Munzīr رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ alieleza, “Mtu mmoja alikuza tabia ya kuwa kimya kwa muda wa miaka 40 kwa kuweka kijiwe mdomoni kwa kiasi kwamba hakukiondoa ila tu anapokula, kunywa na kulala.”

Kumbuka! Jiwe lisiwe dogo mno linaloweza kupita kooni na kusababisha hatari wala lisitiwe mdomoni ikiwa mtu amefunga kwa sababu mchanga nk. waweza kupita kooni.

Tabi'i (Mtu Aliyehubiana Na Swahaba) Aliyekuwa Akijitathmini Mazungumzo Yake Ya Kila Siku

Sayyidunā Rabī' Bin Khušaym رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ hakusema neno lolote la kidunia kwa miaka 20! Kila siku alikuwa akichukuwa kalamu na karatasi akiandika maneno yote alioyasema mchana

ule na ifikapo usiku hurudilia karatasi yake na hujitathmini.

(Iḥyā-ul-‘Ulūm, uk. 137, juz. 3)

Namna Ya Kutathmini Mazungumzo

Kutathmini mazungumzo ni kufikiria kwa makini kila neno linalotamkwa na kuuliza, kwa mfano, “Kwa nini ukasema kadha wa kadha? Ilikuwa na haja gani kuzungumza wakati ule? Ilikuwa na haja gani kuzungumza kwa maneno mengi? Usemi huu, uliosema kwa fulani haukubaliki na sheria na pengine umemuumiza hisia zake-tubu na umuombe msamaha ndugu huyo muislamu. Kwa nini ulikwenda katika mjumuiko huo huku ukijua kuwa kutakuwa na mazungumzo yasiyokuwa na maana na kwa nini uliyapa nguvu? Pia ulisikiliza masengenyo kwa hamu kubwa! Tubia kikweli kweli na uahidi kujiepusha na mjumuiko kama huo.”

Kwa njia hii, mtu mwenye busara aweza kutathmini mazungumzo yake ya kila siku na atayagundua madhambi, uzembe, udhaifu na makosa yake mengi na ataweza kujirekebisha.

Katika mazingira ya Madanī ya Dawat-e-Islami, kujitathmini kunaitwa ‘Fikr-e-Madīnah’ na katika Dawat-e-Islami kunakuzwa fikra ya kufanya Fikr-e-Madīnah angaa kwa dakika 12 kila siku kwa kujaza kijitabu cha Madanī In’āmāt.

‘Umar Bin ‘Abdul ‘Aziz Alia Kwa Shaki

Sayyidunā Abū ‘Abdullāh رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ amesema, “Nimemsikia mwanachuoni mmoja akisema mbele ya Sayyidunā ‘Umar Bin ‘Abdul ‘Azīz رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ “Mwanachuoni mkimya ni kama mwanachuoni msemaji.” Akasema, “Nafahamu kwamba siku ya kiyama mwanachuoni msemaji atakuwa bora ya mkimya kwa sababu ilimu yake itakuwa imefaidi umma, ilhali yule mkimya imemfaidi yeye peke yake.” Halafu mwanachuoni yule akauliza, “Ewe Amīr-ul-Muminīn! Huzijui fitna za kusema?” Aliposikia haya Sayyidunā ‘Umar Bin ‘Abdul ‘Azīz رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ alianza kulia kwa shaki. ((*Aṣ-Ṣamt ma’ Mawsū’ah Ibn-e-Abid-Dunyā, uk. 345, juz. 7, hadith 648*))

Allah عَزَّوَجَلَّ amrehemu na atusamehe sisi kwa Baraka yake bila kufanyiwa hesabu.

أَمِينَ بِجَاهِ النَّبِيِّ الْأَمِينِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ

Maelezo Ya Kisa Hiki

Ndugu wapenzi waislamu! Ajabu iliyoje namna gani watu wema waliotutangulia walivyokuwa na hadhari na ucha Mungu. Bila shaka kwa mwanachuoni mwenye hadhari kuelezea dini ya Allah عَزَّوَجَلَّ, kubalighisha ujumbe wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ na kulingania watu katika wema ni bora kuliko kunyamaza. Walakini maneno ya yule mwanachuoni kwa Sayyidunā ‘Umar Bin ‘Abdul ‘Azīz رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ “Huzijui fitna za kusema?” Ilikuwa

ni sawa na pahala pake; na kulia kwake Amīr-ul-Mūminīn hadi asijifae ni kwa sababu ya kujua undani wa ujumbe huo. Ingawa kuzungumza maneno mazuri kuna faida kwa umma lakini kuna hatari kadhaa kwa msemaji mwenyewe. Kwa mfano, ikiwa mtu ni mlinganizi hodari, basi aweza kughurika na zile sifa anazomiminiwa kwa ajili ya umbuji, ufasaha au kujiona yeye kuwa ana uwezo na ni bora kuliko wengine au kwa kutumia misemo ili kuvutia wengine kwa ajili ya matamano ya kidunia na kujiamini. Ikiwa ni gwiji wa kuzungumza Kiarabu, aweza kujiingiza katika kutumia misemo ya Kiarabu mara kwa mara katika mazungumzo ili kuvutia wengine. Vile vile mwenye sauti nzuri aweza kutawaliwa na kiburi kwa ajili ya kusifiwa na watu akidhani kuwa sauti hiyo nzuri yatokana na juhudi zake badala ya kipawa kutoka kwa Allah عَزَّوَجَلَّ. Kwa hivyo tahadhari kutoka kwa mwanachuoni huyo kuhusu 'kusema' yafaa. Bila shaka mlinganizi mwenye sifa mbaya kama hizo kuzungumza kwake kunaweza kumtia katika fitna kubwa na huenda kukaharibu maisha yake ya ahera hata kama umma ulifaidika na maneno yake.

Tiba Bora Zaidi Ya Kutakasa Mazungumzo Na Maneno Yasiyokuwa Na Maana

Kwa wale ambao wanataka kuchuja mazungumzo yao tiba bora kutoka *Ihyā-ul-'Ulūm* inatolewa hapa kwao ili kusafisha mazungumzo kutokana na maneno yasiyofaa au makosa mengineo. Kulingana na Hujjat-ul-Islam, Sayyidunā Imām

Muhammad Bin Muhammad Bin Muhammad Ghazālī رحمه الله تعالى عليه
“Mazungumzo ni aina nne:

1. Mazungumzo yenye madhara kabisa.
2. Mazungumzo yenye manufaa kabisa.
3. Mazungumzo yenye manufaa na madhara.
4. Mazungumzo yasiyo na manufaa wala madhara.

Kwa hivyo, ni bora kujiepusha na mazungumzo ya aina ya kwanza ambayo yanamadhara tu pekee. Vile vile ni muhimu kujizuia kutokana na mazungumzo ya aina ya tatu ambayo yanamadhara na pia manufaa. Mazungumzo ya aina ya nne yanajumlishwa katika mazungumzo ya upuuzi kwa kuwa hayana manufaa wala madhara. Kwa hivyo kupoteza wakati kuzungumza maneno yasiyo na manufaa wala madhara ni hasara pia. Mazungumzo ya aina ya pili tu ndiyo yaliyobakia kuwa na manufaa yaani robo tatu (75%) ya mazungumzo hayafai ila robo (25%) tu ya mazungumzo ambayo ndiyo yenye faida, ndiyo yanayofaa kutumika. Hata hivyo katika mazungumzo ambayo yanafaa kuzungumzwa kuna hatari ya kuwa na riyaa, kubuni, kusengenya, kutia chumvi, ubaya wa kujivuna yaani kutaja ubora wake na kujitakasa nk. Zaidi ya hayo, kuna hatari ya kuangukia mazungumzo ya upuuzi na kuingia katika mazungumzo ya dhambi. Kwa hivyo katika mazungumzo yenye maana bado mtu yuko katika hatari. ((*Ihyā-ul-'Ulūm*, uk. 138, juz. 3)

Mjinga Husema Bila Ya Kufikiria

Ndugu wapenzi waislamu! Mtu mwekevu (mwenye busara) hupima maneno anayotaka kusema kabla hajayatoa kwenye kinywa chake lakini mjinga huropoka linalomjia kwenye hawaa yake licha ya kuwa litamuibisha. Ndipo Sayyidunā Ḥasan Baṣrī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْعَظِيمِ akasema, “Ilikuwa ni jambo maarufu miongoni mwa watu kwamba ulimi wa mwenye busara hutawaliwa na moyo, kwa sababu huutazama moyo wake kabla ya kuzungumza. (Hutafakari iwapo azungumze au la) Ikiwa linafaida huzungumza (ikiwa ni kinyume) hunyamaza. Kwa upande mwengine moyo wa mjinga hutawaliwa na ulimi, hajasumbui kutafakari yaani linalokuja ulimini hulitoa nje.” (*Tanbih-ul-Ghāfilīn, uk.115*)

Mbinu Ya Kupima (Maneno) Kabla Ya Kusema

Ndugu wapenzi waislamu! Kumbukeni Mtume wetu kipenzi na aliyebarikiwa صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ hata mara moja hakutoa neno la upuuzi kwenye ulimi wake wa kweli uliobarikiwa au kucheka kwa nguvu. Ingekuwa bora iliyoje lau sunnah hizi zingefuatwa!

Mbinu ya kupima maneno kabla ya kuyatoa ulimini ni kujiuliza, “Nazungumza kwa lengo gani?” “Je, nina mlingania mtu yeyote katika mambo mema?” “Je, kuna wema wowote kwangu au kwa mwengine kwa yale ambayo ninataka kusema?” “Je, yale ninayotaka kusema yametiwa chumvi ya kunitia mimi katika dhambi ya kusema urongo?”

Kuhusu mifano ya maneno ya urongo yaliyotiwa chumvi, Şadr-ush-Sharī'ah Badr-ut-Ṭarīqah Mufti Muhammad Amjad 'Alī A'zamī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْقَوِيّ amesema, “Iwapo mtu amekuja mara moja halafu aseme amekuja mara elfu, ni muongo.” (*Bahār-e-Sharī'at*, uk. 519, juz. 3).

Zingatia: “Je, nataka kumpa mtu sifa za uongo?” “Je, nataka kumsengenywa mtu?” “Je, nitamuudhi mtu kwa kusema maneno haya?” “Je, itabidi niombe msamaha baada ya kusema?” “Je, nitatoa siri yangu au ya mwengine?”

Hata baada ya kupima yale unayotaka kusema na ikawa wazi kuwa hayana faida wala hasara na hayana thawabu wala dhambi, bado kuna hasara kwani badala ya kuusumbua ulimi kuzungumza maneno ya upuuzi ni heri ulete dhikri au umswalie Mtume صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ utapata thawabu. Hii ni njia bora ya kutumia wakati: na kukosa faida kubwa kama hii pia ni hasara.

Mbinu Ya Kunyamaza Kimya

Ndugu wapenzi waislamu! Ingawa kuzungumza upuuzi si dhambi, kuna madhara mengi yanayohusishwa nayo kwa hivyo ni muhimu kujizuia kuzungumza upuuzi. Laiti! Laiti! Laiti! tungeweka Qufl-e-Madinah tungekuza tabia ya kunyamaza.

Kisa: Sayyidunā Muwarriq 'Ijlī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى alisema, “Kuna tabia moja nzuri ambayo nilijaribu kuwa nayo kwa miaka 20 lakini bado sijafaulu. Hata hivyo sijavunjika moyo.” Akaulizwa, “Ni tabia gani hiyo?” Akajibu, “Kunyamaza.” (*Az-Zuhd-lil-Imām*

Aḥmad, uk. 310, hadith 1762). Yeyote anayetaka kunyamaza, angaa awasiliane kupitia kuandika au ishara badala ya kutumia ulimi. **إِنَّ شَاءَ اللَّهُ عَزَّوَجَلَّ** Kwa njia hii utaweza kukuza tabia ya kunyamaza. Kwa ajili ya hayo, moja ya Madanī In’āmāt (njia bora ya kumfanya mtu kuwa muongofu) inaeleza, “Je, leo uliweka Qufi-e-Madinah ya ulimi? Ili kuwa na tabia ya kujizuia kuzungumza upuuzi, je, uliwasiliana kwa kutumia ishara au angaa mara 4 kwa kuandika?”

Katika juhudi zako za kujaribu kunyamaza inawezekana kufaulu kujizuia maneno ya upuuzi kwa siku chache lakini halafu tabia ya kuzungumza inaweza kukuregelea tena. Lakini usivunjike moyo, endelea kujaribu tena. Ikiwa juhudi zako ni za dhati basi **إِنَّ شَاءَ اللَّهُ عَزَّوَجَلَّ** bila shaka utafaulu.

Wakati unapofanya mazoezi ya kunyamaza ni bora uwe na tabasamu ili mtu asidhani kuwa umemkasirikia. Wakati huu pia huenda hasira zako zikaongezeka. Mtu asipoelewa, usimkasirikie kwani huenda ukapata dhambi ya kumuudhi. Ni bora tu, kuwasiliana kwa ishara na wale watu ambao una mazoea nao. Mgeni au mtu ambaye huna mazoea naye huenda akaudhika ukiwasiliana naye kwa ishara hivyo basi zungumza nao inapobidi. Bali mara nyingine huwa ni wajib kuzungumza. Kwa mfano kujibu Salamu, ni sunnah kumwamkua mtu kwa kutumia ulimi badala ya ishara. Vile vile mtu akibisha mlango na akaulizwa, “Ni nani huyo?” Basi hafai kusema, “Tafadhali fungua!” Ama “Ni mimi”. Ni Sunnah katika hali kama hiyo kutaja jina lako.

Itaneni Kwa Njia Ya Heshima Ili Mupate Thawabu

Si vizuri kumuita mtu kwa kutumia, “Shish Shish”. Ikiwa unamjua mtu tumia jina lake au Kunniyah yake (kwa jina la mtoto wake kwa mfano babake fulani), kwani kufanya hivyo ni sunnah. Ikiwa humjui mtu kwa jina, kulingana na desturi za mahali hapo, muite kwa heshima. Kwa mfano, mdogo muite “kaka” na mkubwa “mjomba!”

Katika hali yoyote, unapomuita mtu kusudia kupata thawabu kwa kuufurahisha moyo wa muumin. Muite kwa jina lake zima kwa njia nzuri. Kulingana na hali ongeza neno “ndugu” mwisho au “Hajj” kama ameshawahi kuhiji. Anayeitwa naye anafaa kujibu “Labbaik” (nipo).

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَزَّوَجَلَّ Katika mazingira ya Madani ya Dawat-e-Islami, mtu anapoitwa, kawaida hujibu “Labbaik”. Jibu hili ni zuri masikioni na huleta raha katika moyo wa muislamu. Hata Maswahaba رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُمْ walikuwa wakijibu “Labbaik” pindi walipoitwa na Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ.

Tukiongezea, kuna ushahidi kutokana na mfano wa maisha ya Walii wa Allah, kiongozi mkuu wa Mahambali ulimwenguni, Sayyiduna Imama Ahmad bin Hanbal رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ ambapo yeyote aliyekuwa akimuita kumuuliza kuhusu hukumu ya jambo, aliitikia “Labbaik”. ((*Manāqib Imām Aḥmad Bin Hanbal lil-Jawzī, uk. 298*). Imetajwa pia katika kitabu maarufu cha Dua za sunna *Hisn-e-Hasin*, “Mtu yeyote anapokuita, itikia “Labbaik!” (*Hisn Haṣīn, uk. 104*)

Baraka Tatu Zitokanazo na Kunyamaza

1. Kumuona Mtume Mtukufu ﷺ Kwa Sababu Ya Baraka Ya Kunyamza

Huu ni muhtasari wa waraka wa dada muislamu: “Kutokana na kusikiliza hotuba za kuisisimua za sunnah kuhusu faida za kunyamaza kupitia kaseti zinazotolewa na idara ya uchapishaji ya Dawat-e-Islami, Maktaba-tul-Madīnah, nikaanza kufanya mazoezi ya Qufl-e-Madinah (yaani nikaanza mazoea ya kunyamaza). Hazikumalizika siku tatu, niligundua idadi ya maneno yasiyo na maana niliokuwa nikitamka.

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَزَّوَجَلَّ Kutokana na baraka za kunyamaza nikaanza kuota ndoto nzuri nzuri. Katika siku yangu ya tatu ya kujitahidi kujizua kuzungumza ovyo ovyo, nikasikiliza kaseti nyingine ya bayana iliyotolewa na Maktaba-tul-Madīnah iitwayo: ‘What is true Obedience?’

Nilipokwenda kulala usiku huo, اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَزَّوَجَلَّ nikaota kuhusu kisa kilichoelezwa katika kaseti hiyo. Ilikuwa ni vitani, ambapo Mtume رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ anamtuma Sayyidunā Ḥuẓayfah رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ kwenda kuwachunguza maadui. Sayyidunā Ḥuẓayfah alipofika katika mahema ya makafiri, alimuona kiongozi wao Abū Sufyān (alikuwa hapa bado hajasilimu) akiwa amesimama. Aliona hii ni nafasi nzuri, akatoa mshale wake na akauweka kwenye

upinde (tayari kumfuma). Mara akakumbuka amri ya kipenzi Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ “Usichokoze.” Kwa ajili ya utifu wake kwa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ, alijizuia kumfuma mshale. Baadaye akamueleza Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ kuhusu aliyoyaona.

الْحَفْدُ لِلَّهِ عَزَّوَجَلَّ Nilibarikiwa kumuona vizuri Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ pamoja na maswahaba wawili wanaoheshimika رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُمَا; yaliyotokea baadaye siwezi kuyakumbuka vizuri.”

Akaendelea kusema, “Kwa ajili ya juhudi za siku tatu tu za kujizuia kuzungumza mambo ya upuuzi, Mtume wa rehema, Mtetezi wa ummah صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alinijaalia tunu nzuri sana. Sasa ni matamaniao yangu makubwa kuuzuia ulimi wangu kuzungumza upuuzi. Tafadhali niombe ufanisi katika juhudi zangu.”

Kina dada wakiislamu, hasa watamuonea wivu dada huyu aliyebahatika. Ni changamoto kwa mwanamke wa kiislamu kunyamaza kwa sababu wanawake ni wazungumzaji sana kuliko wanaume.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

2. Faida Ya Kunyamaza Katika Kuimarisha Mazingira Ya Madani

Barua fupi iliyotumwa na ndugu muislamu inaeleza: “Pamoja na kuyatilia maanani mazingira ya Madani, nilikuwa mzungumzaji mno na nilikuwa si mswalii Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ kama

inavyohitajika kabla ya kusikiliza hotuba za kulisimua kuhusu kunyamaza katika Ijtimai za Dawat-e-Islami. Lakini tangu nianze kujitahidi kunyamaza, nimebarikiwa kumswalia Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ mara elfu moja kila siku. Nawasilisha zawadi ya swala 12,000 za kumswalia Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ nilizozisoma kwa siku 12 kwako wewe.

Zaidi ya hayo, kuzungumza kwangu sana kulikuwa kukidhuru kazi ya Madani ya Dawat-e-Islami katika Žaīlī Ḥalqāh. Siku chache zilizopita, kulikuwa na Madanī Mashwarāh ili kutatua mzozo. Ajabu! Kwa sababu ya kumyamaza kwangu, اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَزَّ وَجَلَّ ushindani wote ulimalizika!

Nigrān wetu alifurahi mno na akaniambia waziwazi: “Nilikuwa nahofia huenda ukaanza ushindani na kusababisha mazungumzo kusambaratika lakini kwa ajili ya kunyamaza kwako, sote tulijisikia watulivu.” Na ni kweli, zamani hali ya Madanī Mashwarāh ilikuwa ikikoregeka kwa sababu ya tabia yangu ya ubishi na ushindani usio na maana.”

Silaha Ya Madani Kwa Ajili Ya Kazi Za Madani

Ndugu wapenzi waislamu! Je, mumeona ni faida iliyoje kwa kazi ya Madani kujizuia kuzungumza maneno yasiyo na maana! Kwa hivyo mlinganizi wa sunnah awe makini katika kila hali na azungumze kidogo. Akiwa msemaji sana au mwenye kuingilia mazungumzo ya watu wengine au kuzungumza wakati wengine wanazungumza au kuanzisha ubishi na ugomvi basi ipo hatari

kubwa ya kudhurika kazi ya dini kwa ajili yake. Mtu huyu asiye na bahati amenyimwa silaha ya Madani ya kumshinda shetani.

Katika kumpa wasia Sayyidunā Abū Ẓar Ghifārī رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ, Mtume wa ulimwengu, Utulivu wa nyoyo, Karimu na Mwenye huruma صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alisema, “Jilazimishe kuwa mkimya mara nyingi kwani shetani atakimbia kwa (jambo) hili na utapata utulivu katika ulinganizi wa dini.” *((Shu’ab-ul-Īmān, uk. 242, juzuu 4. Hadis 4942))*

3. Faida Ya Kunyamaza Katika Kuimarisha Mazingira Ya Madani Nyumbani

Ndugu wapenzi waislamu! Kwa kuacha tabia ya kuzungumza ovyo ovyo, kucheka na kufanya mzaha, na kutumia maneno yasiyo na adabu, utathaminiwa zaidi nyumbani. Watu wa nyumbani kwako watavutiwa na tabia yako ya umakini. Hapo basi unapowalingania katika mambo mazuri wataathirika haraka na ikiwa mazingira ya Madani hayajajengeka nyumbani kwako, itakuwa rahisi kujengeka.

Kuhusu swala hili, muhtasari wa barua ya ndugu muislamu aliyoandika baada ya kusikiliza hotuba ya kulisimua kuhusu ‘Uboru wa Kunyamaza’ katika Ijtimai ya Dawat-e-Islami ni kama ifuatavyo: “Kwa mujibu wa mafundisho yaliyotolewa kuhusu sunnah, mtu mzungumzaji kama mimi nilianza kujifunza tabia ya kunyamaza. Nimepata faida kubwa mno kutokana na hayo. Watu

nyumbani ambao walikuwa hawaridhiki na mimi tangu nianze kunyamaza, wameanza kunithamini.”

“Hususan, mamangu mzazi, ambaye alikuwa amechoka na mimi, sasa ameridhika sana. Hapo awali nilipokuwa nikizungumza ovyo ovyo, hata maneno yangu mazuri hayakuwa na athari yoyote. Sasa, kila ninapomueleza mamangu kipenzi kuhusu sunnah, hasilikizi kwa makini tu bali pia hujaribu kuitekeleza.

Maua Ya Madani 19 Ya Kuimarisha Mazingira Ya

Nyumbani

1. Ukiingia au ukitoka nyumbani, toa salamu kwa sauti.
2. Ukimuona babako au mamako anakuja, simama kwa heshima.
3. Angalau mara moja kwa siku, ndugu waislamu wa kiume wabusu miguu na mikono ya baba zao na ndugu wakike wabusu miguu na mikono ya mama zao.
4. Zungumza na wazazi wako kwa sauti ya chini, usiwatazame machoni; inamisha kichwa chako chini unapozungumza nao.
5. Papo hapo kamilisha kazi waliyokutuma ikiwa si kinyume na shariah.
6. Kuwa makini. Jizuie kuzungumza ovyo, kuchekacheka, dhihaka, kukasirika kwa ajili ya sababu ndogo, kukosoa

chakula, kuwakemea au kuwapiga ndugu zako wadogo au kubishana na wazee nyumbani. Ikiwa unatabia hizo, lazima ubadili mtazamo wako na umuombe kila mmoja msamaha.

7. Ukiwa na makini nje na ndani ya nyumba **إِنَّ شَاءَ اللَّهُ عَزَّوَجَلَّ** baraka zake zitaingia nyumbani kwako.
8. Zungumza na mamako au mama wa watoto wako (na hata watoto, nje na ndani ya nyumba) kwa heshima.
9. Yasipite masaa mawili baada ya swala ya jamaa ya Isha msikitini uwe ushalala ili uweze kuamka usiku kuswali swala ya Tahajjud au angalau kuswali swala ya asubuhi ya jamaa kwa urahisi katika safu ya mwanzo. Pia usipate uchovu kazini (siku ya pili).
10. Ikiwa watu nyumbani ni wavivu kuswali au ikiwa wanafanya dhambi kwa kutojihifadhi kuangalia filamu na drama au kusikiza nyimbo na wewe si kiongozi wa nyumba na zaidi unaamini kuwa kuna uwezekano wa wao kutosikiliza ushauri wako, basi tumia maneno mazuri kuwahimiza kusikiliza au kutazama kaseti au CD za bayana (hotuba) za Maktaba-tul-Madīnaḥ na uwahimize kutazama idhaa ya Madani. **إِنَّ شَاءَ اللَّهُ عَزَّوَجَلَّ** Utaona matokeo ya kutia moyo.
11. Kuwa na subira! Kuwa na subira! Kuwa na subira hata kama utakemewa namna gani au kupigwa nyumbani. Ikiwa utalipiza kisasi basi utaondoka uwezekano wa kupatikana mazingira ya Madani nyumbani.

12. Njia moja ya kukuza mazingira ya Madani nyumbani ni kusikiliza darsa kutoka Faizan-e-Sunnat kila siku.
13. Waombe kwa dhati watu nyumbani du'a mara kwa mara ya kupata wema wa duniani na akhera kama alivyosema kipenzi chetu Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ. **الدُّعَاءُ سِلَاحُ الْمُؤْمِنِ**. "Du'a ni silaha ya muumin." (*Al-Mustadrak lil-Hākim, uk. 162, juzuu 2, Hadis 1885*)
14. Mke achukulie nyumba ya mumewe kuwa ni 'nyumba yake' na wakweze kuwa ni wazazi wake. Awafanyie wema kama anavyowafanyia wazazi wake kwa kuzingatia mipaka ya sheria. Mke asibusu miguu au mikono ya bevyaa (babake mumewe). Vile vile mume asibusu miguu au mikono ya mamkwe (mamake mkewe).
15. Imetajwa katika Masail-ul-Qur'an ukurasa wa 290, "Soma du'a ifuatayo baada ya kila swala (pamoja na kumswalia Mtume mara moja kabla na baada yake) اِنْ شَاءَ اللهُ عَزَّوَجَلَّ watu wa nyumba yako watashikamana na sunnah zilizobarikiwa na mazingira ya Madani yatakua nyumbani kwako:

[اَللّٰهُمَّ] رَبَّنَا هَبْ لَنَا

مِنْ اَزْوَاجِنَا وَذُرِّيَّتِنَا قَرَّةَ اَعْيُنٍ وَاجْعَلْنَا لِلْمُتَّقِيْنَ اِمَامًا ﴿٢٧﴾

¹ Na wale wanaosema, " Mola wetu! Tupe katika wake zetu na watoto wetu yaburudishayo macho (yetu) (nyoyo zetu) na utujaalie kuwa waongozi kwa wamchao (Mungu)." (*Part 19, Sura Furqan 74*)

16. Msomee mtoto au mtu mzima ambaye ni mtovu wa adabu kichwani wakati amelala aya hii mara moja kwa siku 11 au 21 kwa sauti isiyoweza kumuamsha:

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

بَلْ هُوَ قُرْآنٌ مَّجِيدٌ ﴿٦٦﴾ فِي نُوحٍ مَّحْفُوظٍ ﴿٦٧﴾

(Mswalie Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ kabla na baada ya kusoma aya hiyo) Kumbuka! Ikiwa ni mtu mzima ambaye si mtiifu na kwa kusoma dua hii kichwani mwake huenda akaamka hasa kama hana usingizi mzito basi asisomewe kisomo hiki. Hususan mke kwa mumewe (yaweza kusababisha ugomvi).

17. Ili kuwafanya watoto wasiokuwa watiifu kuwa watiifu, soma يَا شَهِيدُ mara 21 kila siku baada ya swala ya asubuhi huku uso wako ukiuelekeza mbinguni mpaka ulitakalo ulipate. (Mswalie Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ kabla na baada yake)

18. Ishi kulingana na Madanī In'āmāt. Wabembeleze watu wa nyumbani kwako wenye nyoyo laini kwa hekima na upole kufuata Madanī In'āmāt. Baba ajitahidi kuwafanya watoto wake watekeleze Madanī In'āmāt kwa busara na upole. Kutokana na ukraimu wa Allah عَزَّوَجَلَّ mabadiliko ya ki Madani yatatokea nyumbani.

¹ Bali hii ni Qurani tukufu. (Iliyotolewa) katika huo ubao uliohifadhiwa, (wa Mwenyezi Mungu).
(Part 30, Sura Buruj: 74)

19. Safiri pamoja na wafuasi wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ katika Madanī Qāfilāh angalau kwa siku 3 na uwaombe watu wa familia yako du'a. Kutokana na baraka za Madanī Qāfilāh, nyumba nyingi zimebadilishwa kuwa na mazingira ya Madani.

Ndugu wapenzi waislamu! Kufikia mwisho wa hotuba yangu, nachukua fursa hii kuwaeleza kuhusu baadhi ya sunnah na adabu za Kipenzi chetu Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ ambaye amesema, “Anayeipenda sunnah yangu, ananipenda mimi na anayenipenda mimi atakuwa nami peponi.” (*Ibn 'Asākir, uk. 343, juzuu 9*)

20 Faida Za Madani Kuhusu Mswaki

Zingatieni hadithi mbili za Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ kuhusu mswaki:

1. Rakaa mbili zilizoswaliwa baada ya kupiga mswaki ni bora mara 70 kuliko zile ambazo zimeswaliwa bila kupiga mswaki. (*Attarghīb Wattarhīb, uk. 102, juzuu 1 Hadis 18*)
2. Jilazimisheni kupiga mswaki kwani ndani yake kunapatikana usafi wa meno na ni sababu ya kupata radhi za Allah عَزَّوَجَلَّ. (*Musnad Imam Ahmad, uk. 438, juzuu 2 Hadis 5869*)
3. Katika ukurasa wa 288, juzuu ya kwanza ya Bahar-e-Shariat, iliyochapishwa na Maktaba-tul-Madinah, idara ya uchapishaji ya Dawat-e-Islami, Allamah Maulana Mufti

Muhammad Amjad ‘Ali A’zami عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْقَوِيّ amesema, “Wanavyuoni wakuheshimika wanasema kwamba yeyote mwenye mazoea yakupiga mswaki, atabirikiwa na bahati ya kupiga shahada wakati mauti yakimjia na yeyote anayetumia madawa ya kulevya hatojaaliwa kupiga shahada wakati wake wa kukata roho.”

4. Imeelezwa kutoka kwa Sayyidunā Ibn ‘Abbās رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهُ kuwa mswaki una faida kumi: Unasafisha mdomo, unayapa nguvu masine, unayapa nguvu macho, unaondoa kohozi, unaondoa harufu mbaya ya mdomo, ni sunnah, malaika hufurahi, Allah عَزَّوَجَلَّ huridhika, huongeza amali njema na hurekebisha tumbo. (*Jam’-ul-Jawāmi’ lis-Suyūfī, uk. 249, juzuu 5 Hadith 14867*)
5. Sayyidunā ‘Abdul Wahhāb Sha’rānī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْقَوِيّ anaeleza, “Wakati mmoja Sayyidunā Abū Bakr Shibli Baghdadi عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْهَارِيّ alipokuwa akitawadha, alikuwa na haja ya mswaki na akatafuta lakini hakupata. Kwa hivyo akanunua mswaki kwa dinar moja (sarafu ya dhahabu) na akaupiga. Watu wakamuuliza, “Umetumia pesa nyingi kununua mswaki! Je mtu afaa kutumia pesa zote hizo kwa ajili ya mswaki? Akajibu, “Bila shaka, ulimwengu wote huu pamoja na vilivyomo ndani hauna hata thamani ya ubawa wa mbu mbele ya Allah عَزَّوَجَلَّ. Nitajibu nini ikiwa Allah عَزَّوَجَلَّ ataniuliza Siku ya Hukumu, “Kwa nini uliziacha sunnah za Kipenzi changu? Thamani ya pesa na mali niliyokupa haifikii hata thamani ya ubawa wa mbu mbele

yanu. Basi kwa nini usitumie mali hiyo yenye kustahili kudharauliwa kutimiza sunnah kubwa (kupiga mswaki)?
(Lawaqah-ul-Anwar, uk. 38)

6. Sayyidunā Imām Shāfi’ī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْقَوِيّ amesema, “Mambo manne yanaimarisha uwezo wa kufikiri: kujizuia na porojo, kutumia mswaki, kujihusisha na wacha Mungu na kufuata elimu ya dini uliyonayo.”
7. Mswaki uwe ni wa mti wa mzaituni au mwarobaini au mti wowote ambao ni uchungu.
8. Unene wa mswaki uwe sawa na kidole kidogo.
9. Urefu wa mswaki usipite shubiri moja ya mkono la sivyo shetani huukalia.
10. Ncha ya mswaki iwe laini la sivyo, yaweza kusababisha kutengana kwa meno na masine.
11. Mswaki mbichi ndiwo mzuri; aidha uiweke kwenye glasi ya maji mpaka uwe laini.
12. Ichonge ncha ya mswaki kila siku kwa sababu inafaida tu ikiwa inauchungu uchungu.
13. Piga meno mswaki kuelekea kulia- kushoto au kushoto-kulia.
14. Daima piga mswaki kwa mizunguko mitatu.

15. Osha mswaki baada ya kila mzunguko.
16. Ushike mswaki kwa mkono wa kulia kwa namna ambayo kidole kidogo kiko chini yake, vidole vitatu vya katikati viko juu yake na kidole gumba kimeelekea kwenye ncha (sehemu ambayo hutumika kusafisha meno).
17. Kwanza piga mswaki meno ya juu ya kulia halafu ya juu ya kushoto. Kisha piga meno ya chini ya kulia halafu ya chini ya kushoto.
18. Ukiushika mswaki kwa ngumi inahatarisha kupata maradhi ya bawasili (maradhi ya tumbo).
19. Kupiga mswaki ni sunnah inayofuata udhu lakini ikiwa mmoja anaharufu mbaya (ya mdomoni) basi inakuwa ni sunnah iliyokokotezwa. (*Fatawa Razawiyyah (Jadid), uku. 623, vol. 1*)
20. Usiutupe mswaki uliotumika au ncha yake kwa sababu ni kitu cha kutekeleza sunnah bali uweke mahali pazuri, uzike au utie baharini. (*kwa habari zaidi kuhusu mswaki rejelea Bahar-e Shariat, uk. 294-298 juzuu 1 kilichochapishwa na Maktaba-tul-Madinah*)

Ili upate kujifunza sunnah nyingi, nunua vitabu viwili vya Maktaba-tul-Madinah: (i) Bahar-e-Shariat sehemu ya 16 chenye kurasa 312. (ii) Sunnatayn aur Adab chenye kurasa 120. Njia bora ya kujifunza sunnah ni kusafiri pamoja na (sunnah zenye kuisimua) Madani Qafilah wa Dawat-e-Islam.

Amali Inayosababisha Kupungua Kwa Adhabu

Ndugu wapenzi waislamu! Mola عَزَّوَجَلَّ akimteremshia mja wake rehema, hutakabali hata amali ndogo na humsamehe.

Sayyidunā ‘Abdur Raḥmān Bin Samurāḥ رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ aeleza kuwa siku moja Mtume wa ulimwengu, amani ya nyoyo, karimu mno na mwenye huruma صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alitujia na akasema, “Jana usiku niliota, niliona:

1. Malaika wa mauti عَلَيْهِ السَّلَام alikuja kuitoa roho ya mtu, lakini utiifu wake kwa wazazi ulikuja mbele yake na kumuokoa.
2. Mtu mmoja aliyekuwa akipata adhabu kaburini aliokolewa na tabia yake nzuri ya kutawadha.
3. Mtu mmoja alikuwa amezingirwa na mashetani lakini tabia yake ya kumtaja Mwenyezimungu عَزَّوَجَلَّ ilimuokoa.
4. Mtu mmoja alikuwa amezingirwa na malaika wa kutoa adhabu bali swala zake zikamuokoa.
5. Mtu mmoja ulimi wake ulikuwa ukining’inia kwa sababu ya kiu, alikaribia ziwa la maji ili anywe lakini hakuruhusiwa, halafu saumu ikamjia na kuizima kiu yake.
6. Mtu mmoja alijaribu kuwakaribia Mitume عَلَيْهِمُ السَّلَام lakini hakuruhusiwa, ghusul (josh lake) likaja na kumkalisha karibu nami (karibu na Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)

7. Mtu mmoja alijawa na hofu kwa sababu ya kuzungukwa na giza kuu lakini Hajji na Umrah zilikuja na kumtoa gizani na kumpeleka katika mwangaza.
8. Mtu mmoja alizungumza na waislamu lakini hawakumsikiliza. Halafu tabia yake njema kwa jamaa zake ikawaomba waislamu kumsikiliza, basi wakaanza kuzungumza naye.
9. Mtu mmoja alitumia mikono kujikinga kutokana na moto uliokuwa unamjia machoni na mwilini lakini sadaka zake zikaja na kuwa ngao yake.
10. Mtu mmoja alikuwa amezingirwa na Malaika wa adhabu lakini tabia yake njema ya kulingania watu katika njia ya haki na kuwakataza kutenda maovu ilimuokoa na kumpeleka kwa Malaika wa rehema.
11. Mtu mmoja alikuwa amekaa kitako cha tahiyatu lakini kulikuwa na kizuizi kati yake na Allah عَزَّوَجَلَّ, halafu tabia yake njema ikaja na kumkutanisha na Allah عَزَّوَجَلَّ
12. Mtu mmoja alikuwa tayari kupewa kitabu chake cha amali kwa mkono wa kushoto lakini uchaji wake wa Allah عَزَّوَجَلَّ ulikuja na kumnusuru na akapewa kitabu kwa mkono wa kulia.
13. Uzito wa thawabu za mtu zilikuwa nyepesi mno kuliko madhambi yake lakini ukarimu wake ulikuja na kuongeza uzito wa thawabu zake.

14. Mtu mmoja alikuwa amesimama kwenye ukingo wa Jahanamu lakini uchaji wake wa Allah ﷺ ulikuja kumuokoa.
15. Mtu mmoja alianguka katika moto wa Jahannam lakini machozi aliyotoa kwa ajili ya kumcha Allah ﷺ alikuja kumuokoa.
16. Mtu mmoja alikuwa amesimama katika Sirat (daraja jembamba kama uzi lilonyooka) huku anatetema kama tawi la mti lakini kwa kuwa alikuwa na matumaini kwamba Mwenyezimungu ﷺ atamrehemu, rehema za Mwenyezimungu zilimjia na kumuokoa kuvuka daraja.
17. Mtu mmoja alikuwa anatambaa katika Sirat (daraja jembamba kama uzi lilonyooka), swala alizokuwa akiniswalia mimi (Mtume ﷺ) zilimwezesha kusimama na kuvuka daraja hilo.
18. Mmoja wa wafuasi wangu alifikia mijilango mikubwa ya peponi lakini ilikuwa imefungwa lakini ushahidi wake, “Hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah ﷺ ulikuja na Mijilango ya peponi ikafunguka na kumruhusu kuingia.

صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ

Msamaha Kwa Aliyeabudu Moto

Kulikuwa na mtu mmoja akiishi Bukhara ambaye anaabudu moto. Siku moja alikuwa akitembea soko la waislamu pamoja na mwanawe wa kiume. Mwanawe akaanza kula hadharani. Alipomuona mwanawe akila, alimpiga kibao na kumkemea; “Huoni haya kula hadharani katika soko la waislamu katika mwezi wa Ramadhani?” Mtoto akajibu, “(Lakini) Baba, si hata wewe pia huwa wala katika mwezi wa Ramadhani au sio? Baba akajibu, “Mimi huwa sili mbele ya (macho) waislamu. Mimi hula nyumbani ambapo hawawezi kuniona. Mimi si uvunjii heshima mwezi Mtukufu wa Ramadhan” Baada ya muda, mwabudu huyu wa moto alifariki. Mtu mmoja alimuota. Katika ndoto, alimuona akitembea peponi. Alishangaa na kuuliza, “Wewe ulikuwa ukiabudu moto, uliingiaje peponi? Akajibu (mwabudu moto), “Ni kweli nilikuwa nikiabudu moto lakini wakati wa mauti, Mola ﷺ alinibariki na akanijaalia imani kwa kuuheshimu mwezi wa Ramadhan na akaniridhia pepo baada ya kufariki.” *(Nuzha-tul-Majalis, uk.217, toleo la 1)*

Rehema za Allah ﷺ ziwateremkie nasi tusamehewe kwa baraka zao.

صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ

Baraka Za Sunnah

الحمد لله Katika mazingira ya Dawat-e-Islami (shirika la harakati ya Quran na Sunnah la kimataifa lisilo jihusisha na siasa) tuna funza na kufundisha Sunnah za Bwana Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ. Hudhuria ijtimai ya kila wiki siku ya al-khamis baada ya sala ya magrib inayofanyika katika mji wako. Safiri pamoja na wapenzi wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ katika Madani Qafilah na uweke azma yakujaza kadi ya zawadi 72 za Madina (Madani In'amaat) na kumkabidhi msimamizi (Zimmedaar) kila mwezi. Kwa Baraka ya kufanya hivi بِإِذْنِ اللَّهِ تَعَالَى tutzaweza kushikamana na Sunnah za Bwana Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ na tutachukia maasi na tutaweza kulinda imani yetu.

Kila moja aweke azma hii "Ninataka kusuluhisha nafsi yangu na watu wa ulimwengu mzima بِإِذْنِ اللَّهِ تَعَالَى". Kusuluhisha nafsi yangu nita fuata "Madani In'amaat" na kusuluhisha nafsi za watu wa ulimwengu mzima nita safiri katika "Madani Qafilah" بِإِذْنِ اللَّهِ تَعَالَى.

